

athari ya kudidimia uchapishaji nchini tanzania na ukuaji wa kiswahili

Abdullah Saiwaad

Readit Books Ltd.

Barua pepe: readitbook@gmail.com

Simu: +255655286406

Faksi: +255222666424

MAKALA HII ILIWASILISHWA KATIKA KONGAMANO LA PILI LA
KIMATAIFA KISWAHILI 2018 – 12 -13 DESEMBA 2018 UKUMBI WA
SHEIKH IDRIS ABDUL WAKIL

UTANGULIZI

Kiswahili ni lugha ya Taifa ya Tanzania. Kimsingi mawasiliano yote baina ya Watanzania huwa katika lugha ya Kiswahili. Mawasiliano huweza kufanyika ana kwa ana katika mazungumzo au kwa kutumia maandishi. Kwa kutumia maandishi si tu unawasiliana bali unaweka na kumbukumbu. Vilevile kuna uhusiano wa moja kwa moja baina ya uwepo na ukuaji wa lugha na uwepo wa maandiko ya kudumu katika lugha husika. Aghalabu maandiko ya kudumu huwekwa kwenye vitabu. Iwe vitabu vinavyotengenezwa na karatasi au vinginevyo.

Ni dhahiri kuwa ukuaji wa sekta ya vitabu Tanzania hauendani na ukuaji wa idadi ya watu na ukuaji wa sekta zingine za uchumi nchini. Hakika kuna ishara zinaonesha kuwa sekta hii kwa ujumla imeshuka mfululizo kuanzia miaka ya sabini, ilianza kupanda katika miaka kati ya 1993 hadi 2013 na kwa sasa inashuka kufikia viwango chini ya vile vilivyokuwa vimefikiwa mwaka 1993.

Sababu za kushuka kwa ukuaji wa tasnia ni nyingi na zinahusisha mabadiliko ya siasa na jamii pamoja na sababu za kiuchumi. Kuanguka kwa uchumi katika miaka ya 1970, ni moja ya mfano wa sababu hizo. Kukosekana kwa uchapishaji, uchapaji na mfumo wa usambazaji ulioendelea wakati wa uhuru pia ni moja ya tatizo. Kiwango cha chini cha ufanisi katika elimu na lugha miongoni mwa Tanzania ni kitu ambacho pia

kinachangia kutokuwepo sekta iliyoendelea.

Lakini juu ya yote, mfumo wa kiseru ya serikali ambao katika miaka ya 1960 ulioachia biashara ya uchapishaji na usambazaji wa vitabu vya kielimu kwa ukiritimba wa mashirika ya umma pekee, ulikaba koo mfumo dhaifu wa usambazaji wa vitabu wa sekta binafsi. Miaka ya tisini, uliona sera mpya zilizohusisha sekta binafsi katika uchapishaji na usambazaji wa vitabu vya kielimu. Kipindi hiki sekta ilionekana kupanda kwa ufanisi. Hata hivyo kuanzia mwaka 2010, ukabadilika tena na ikawa kengele inayolizwa kuashiria msiba – wa sekta ya vitabu.

Vitendo vya serikali kupitia sera hasi vimekuwa ni nyenzo ya kurudisha nyuma ukuaji wa sekta ya vitabu. Kwa wakati mwingine maamuzi ya serikali ya kuweka sera chanya na wezeshi huwa ufunguo wa kufufua na kukuza sekta ya vitabu. Mabadiliko haya ya kujirudiarudia ya sera imechangia mfululizo katika kudumaa kwa biashara ya vitabu Tanzania.